

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Zanzibar
05 Machi, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RAIS SAMIA AAGIZA SEKTA YA NISHATI ISIMAMIWE VIZURI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema sekta ya nishati ina uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo ya uchumi na maisha ya kila siku ya mwanadamu.

Rais Samia amesema ni lazima wanaosimamia sekta hiyo wahakikishe wanatimiza wajibu wao kwa uzalendo mkubwa na wajitahidi kuzingatia kanuni zote za utunzaji wa mitambo na miundombinu inayotoa nishati ili iwe kwenye hali nzuri wakati wote.

Rais Samia ametoa maagizo hayo kwa Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania-(TANESCO) pamoja na Wakala wa Umeme Vijijini (REA), wakati wa hafla ya uapisho wa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. James Peter Mataragio, Ikulu Ndogo Tunguu.

Aidha Rais Samia ametaka kuwepo na mwendelezo wa utoaji wa taarifa wa mara kwa mara ndani ya Serikali na kwa umma iwapo kuna matengenezo au hitilafu ili ijulikane na kuepusha manung'uniko yanayosababishwa na kutokuwa na taarifa.

Kuhusu gesi Rais Samia ameitaka Wizara hiyo kuhakikisha inatengeneza mpango maalum wa usambazaji wa gesi ili iwe rahisi kualika sekta binafsi iweze kushirikiana nao na hivyo kufikia lengo lililokusudiwa la 85% ya kaya ziwe zinatumia nishati safi ifikapo mwaka 2031.

Pia Rais Samia amesema zipo nchi zilizoonesha nia ya kufanya kazi na Tanzania katika masuala ya gesi hivyo ni muhimu kuangalia sheria na miongozo inayoifunga Serikali kukaribisha sekta binafsi na kufanyia marekebisho.

A handwritten signature in blue ink.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu